**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

**Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,**

**Baraza la Madiwani.**

**TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA – DISEMBA) MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWENYE KIKAO CHA TAREHE 27/02/2023**

## 1.0. UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti***, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii itagusa Maeneo yafuatayo:-

i. Taarifa ya Maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara
ii. Taarifa ya Makusanyo kwa robo ya pili.
iii. Taarifa ya fedha za mapato ya ndani zilizopelekwa kwenye miradi ya Maendeleo
iv. Taarifa ya Uzinduzi wa Madarasa 110 yaliyogharimu Tsh. 2.2 Bilioni, na ugawaji wa vishkwambi 1,190.
v. Taarifa ya ziara ya mafunzo ya Waheshimiwa Madiwani na Wataalam kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Singida Tarehe 26/10/2023.



CamScanner

vi. Taarifa ya Ziara ya Mafunzo ya Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Ilemela katika Jiji la Arusha na Manispaa ya Moshi Mwezi Disemba 2022.
vii. Taarifa ya kukabidhi madawati kwaajili ya shule za Msingi
viii. Taarifa ya Mtihani wa Darasa la Saba 2022
ix. Taarifa ya Mtihani wa kidato cha Nne kwa kwaka 2022

## 2.0. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI.

i. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mnamo Tarehe 09/12/2022, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela iliungana na Watanzania wote katika kuadhimisha maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania bara yaliyokuwa na kaulimbiu isemayo "AMANI NA UMOJA NI NGUZO YA MAENDELEO YETU". Maadhimisho haya yalianza tarehe 02 Desemba, 2022 hadi tarehe 09 Desemba, 2022. kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo Bonanza la Michezo, Kongamano, Shughuli za usafi wa mazingira, na upandaji miti katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri yetu na kuhitimishwa kwa kongamano lililojadili mada iliyohusu **Maendeleo ya Tanzania baada ya Uhuru.**

ii. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Hadi kufikia Disemba mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri imefanikiwa kukusanya jumla ya TSh. 9,433,842,484.00 sawa na asilimia 70 ya makisio ya bajeti ya mwaka 2022/2023 ambayo ni mapato ya ndani, kati ya hayo mapato halisi ni Tsh. 4,623,383,233.00 sawa na asilimia 35.6 ya bajeti, mapato fungwa ni Tsh. 151,349,995 sawa na asilimia 27 ya bajeti na 4,659,109,256.00 ni mapato yaliyotokana na mauzo ya viwanja.

iii. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kwa robo ya pili, kiasi cha shilingi **1,146,470,929.84** zilielekezwa kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ufuatao:

**Elimu Msingi**

- Ukamilishaji wa darasa na ofisi 1ya mwalimu Shule ya Msingi Kiseke Tsh. 12,500,000.00
- Malipo ya pango la ardhi kwenye eneo lilikotolewa na kanisa kwaajili ya Ujenzi wa Shule ya Msingi Kata ya Nyasaka Tsh. 4,523,650.00
- Ujenzi wa matundu ya vyoo shule ya Msingi Ibungilo Tsh. 10,000,000.00
- Ujenzi wa bweni kwaajili ya watoto wenye mahitaji Maalum Shule ya Msingi Buswelu Tsh. 3,190,000.00
- Ununuzi wa eneo la Ujenzi wa Shule ya Msingi Kata ya Kahama Tsh. 2,000,000.00
- Ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule ya msingi Kangaye Kata ya Nyakato Tsh. 15,000,000.00
- Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi ilioko katika Kata ya Kahama 50,000,000.00

**Jumla Ndogo Elimu Msingi ni Tsh. 97,213,650.00**

**Afya**

- Ujenzi wa wodi ya mama na mtoto kituo cha Afya Buzuruga Tsh. 85,000,000.00
- Ujenzi katika Hospitali ya Wilaya Tsh. 17,068,115.5
- Matengenezo katika chumba cha X-RAY Kituo cha Afya Karume Tsh. 3,939,057.44
- Ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba za watumishi Kituo cha Afya cha Sangabuye Tsh. 2,885,500.00
- Ujenzi wa jengo la kujifungulia akina mama Zahanati ya Nyamwilolelwa Tsh. 25,000,000.00
- Kuweka mtandao wa maji katika Kituo cha magonjwa ya mlipuko Buswelu Tsh. 3,487,648.00

**Jumla ndogo Afya ni Tsh. 137,380,320.94**



CamScanner

**Utawala**

- Ukamilishaji wa Jengo la Utawala Tsh. 175,657,079.34
- Ujenzi wa Ofisi ya Mtaa wa Nyamiswi Kata ya Sangabuye Tsh. 15,077,075.00

**Jumla Ndogo Utawala ni Tsh. 190,734,154.34**

**Biashara Viwanda na Uwekezaji**

- Mradi wa Tofali Tsh. 87,674,960.00
- Ununuzi wa vifaa vya Umeme Stendi ya Nyamhongolo Tsh. 4,740,000.00
- Uwekaji Mfumo wa majitaka Soko la muda la Magomeni Tsh. 3,281,675.00
- Matengenezo ya genereta soko la Kirumba Mwaloni Tsh. 990,000.00

**Jumla ndogo Biashara Viwanda na Uwekezaji ni Tsh. 96,686,635.00**

**Miundombinu, Maendeleo ya Miji na Vijiji**

- Ufunguaji wa barabara ya mradi wa viwanja vya Nyafula zenye urefu wa kilometa 59 Tsh. 56,459,207.00
- Kupasua mawe katika barabara ya Kazamoyo Tsh. 3,500,000.00

**Jumla Ndogo Miundombinu, Maendeleo ya Miji na Vijiji ni Tsh. 59,959,207.00**

**Mipango miji**

- Katika Mradi wa Upimaji wa viwanja vya Nyafula, idadi halisi ya viwanja vilivyopimwa ni **3,255.** Kati ya hivyo, viwanja 3,065 tayari vimeuzwa na jumla ya Tsh. **4,659,109,256.00** imekusanywa. Viwanja vilivyobaki ni 190. Fedha zinazodaiwa (Madeni) ni Jumla ya shilingi 7,811,375,414.06
- Jumla ya Ulipaji wa Fidia kwa kipindi hiki ni **Tsh. 279,496,963.50**.

**Maendeleo ya Jamii**

- Jumla ya fedha iliyopelekwa kwenye Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ni **Tsh. 285,000,000.00** kwa jumla ya vikundi 37. Kati ya hivyo, vikundi vya Wanawake ni 28 vilivyopokea Tsh. 228,000,000.00



CamScanner

Vikundi vya Vijana ni vikundi 07 vilivyopokea kiasi cha Tsh. 53,000,000.00 na vikundi vya Watu wenye Ulemavu ni vikundi 02 vilivyopokea kiasi cha Tsh. 4,000,000.00

Vilevile katika makusanyo yanayotokana na marejesho ya vikundi (revolving fund) tumefanikiwa kununua bajaji 1 na kukabidhiwa mtu mwenye ulemavu wa kata ya Pasiansi yenye thamani ya Tsh. 8,100,000,000.00.

iv. ***Mheshimiwa Mweyekiti,*** Mnamo Tarehe 22/12/2022 Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima alizindua rasmi vyumba vya madarasa 110, na seti 5,500 za meza na viti yaliyogharimu TSH. 2,200,000,000.00 fedha kutoka Serikali Kuu. Madarasa hayo yamejengwa kwenye shule 23 za Sekondari zilizopo katika Halmashauri yetu. Sambamba na hilo, alizindua rasmi matumizi ya vishkwambi 1,190 na kuvikabidhi kwa waalimu wa shule za Msingi na Sekondari, Maafisa Elimu Ngazi ya Kata na Maafisa Elimu katika Manispaa ya Ilemela.

v. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo tarehe 26/10/2022 Wahe, Madiwani na Wataalam kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Singida walifika katika Halmashauri yetu ambapo walibadilishana uzoefu juu ya masuala mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa mapato, usafi wa mazingira na pia walipata fursa ya kutembelea Stendi ya Mabasi na Malori Nyamhongolo.

vi. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo Mwezi Disemba 2022 Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa yetu walitembelea katika Halmashauri ya jiji la Arusha ambapo walipata fursa ya kutembelea na kujifunza baadhi ya miradi ikiwemo Mradi wa Uzalishaji wa Protini na chakula cha Mifugo, Mradi wa Dampo la Kisasa, na Mradi wa Kiwanda cha Nyama cha Arusha Meat Company Limited. Pia walitembelea Manispaa ya Moshi ambapo walijifunza namna nzuri ya kudhibiti taka ngumu, na utunzaji mzuri wa mazingira.



CamScanner

vii. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo Mwezi Oktoba 2022, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela aliikabidhi Halmashauri yetu madawati 710 ambayo yalikabidhiwa kwa shule 33 za msingi, Vilevile Meneja wa Benki ya NBC- Mwanza alikabidhi madawati 50, na Meneja wa Stanbic- Mwanza alikabidhi madawati 60 na kufanya idadi ya madawati iliyokabidhiwa katika Halmashauri yetu kwa kipindi hiki kufikia 820.

viii. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo Mwezi Oktoba 2022 Jumla ya wanafunzi 13,340 wa shule za Msingi za Halmashauri yetu, walifanya mitihani ya kuhitimu Elimu ya msingi katika shule za msingi 76 za serikali na 44 za Binafsi. Aidha, kwa mwaka 2022, Halmashauri imepata ufaulu kwa asilimia 96. na kushika nafasi ya 2 Kimkoa na 6 Kitaifa katika mtihani wa darasa la saba.

ix. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** mnamo Mwezi Novemba 2022 Jumla ya wanafunzi 7,378 wa shule za Sekondari katika Halmashauri yetu, walifanya mitihani ya kuhitimu Elimu ya Sekondari katika vituo 26 vya Serikali na vituo 22 vya Binafsi.

***Mheshimiwa Mweyekiti,*** naomba kuwasilisha.

Eng: Modest J. Apolinary

**MKURUGENZI WA MANISPAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



CamScanner